**TAARIFA YA HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI KATIKA MKOA WA RUKWA KWA MHESHIMIWA MKUU WA MKOA WA RUKWA ZELOTE S.ZELOTE SIKU YA UZINDUZI WA HUDUMA ZA UZAZI KATIKA KITUO CHA AFYA MAZWI NA UGAWAJI WA VIFAA VYA UZAZI KWA AJILI YA VITUO VYA HUDUMA ZA AFYA MKOA WA RUKWA TAREHE 27 JULAI 2017**

- Mheshimiwa Mgeni Rasmi Mkuu wa Mkoa wa Rukwa
- Katibu Tawala wa Mkoa
- Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Rukwa
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya
- Waheshimiwa Wabunge
- Mstahiki Meya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga
- Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri
- Wajumbe wa sekretariet ya Mkoa na wataalam wote kutoka Ofisi ya Mkoa
- Makatibu Tawala wa Wilaya
- Wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Rukwa
- Waganga wakuu wa Halmashauri
- Mwenyekiti wa Bodi ya Afya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga
- Wajumbe wa kamati ya uendeshaji wa huduma katika kituo cha Afya Mazwi
- Wataalamu wote kutoka ngazi ya Wilaya na taasisi
- Watendaji wa kata
- Wananchi wote

- Waandishi wa habari
- Mabibi na mabwana

*HABARI ZA ASUBUHI…..*

**Mheshimiwa Mgeni rasmi**,kwanza napenda kuchukua fursa hii,kwa niaba yako kuwakaribisha wote waliofika hapa leo kwa ajili ya kushuhudia tukio muhimu sana la ugawaji wa vifaa tiba kwa ajili ya huduma za afya ya uzazi katika Mkoa wetu wa Rukwa tukio litakalokwenda sambamba na uzinduzi wa huduma za uzazi (Kujifungua) katika Kituo cha afya Mazwi.

**Maelezo mafupi kuhusu hali ya huduma za afya ya uzazi na mtoto katika Mkoa wa Rukwa**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Mkoa wa Rukwa una jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 219, ambapo kati ya hivyo, vituo 202 (92%) vinatoa huduma za uzazi.

**Mheshimiwa Mgeni rasmi**, kwa mwaka 2016, jumla ya akina mama wajawazito 161,089 walihudhuria huduma za kliniki ya wajawazito na katika vituo vya kutolea huduma za afya.Jumla ya akina mama waliojifungua na taarifa zao kupatikana ni akinamama**43,938** na kati ya hao, akina mama **41,698** (95%) walijijifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya na akina mama **2,240**(5%) walijijifungulia nje ya vituo vya kutolea huduma kwa sababu mbalimbali

**Mheshimiwa Mgeni rasmi**, kati ya akina mama wote waliojifungulia katika vituo vya huduma ndani ya Mkoa, akina mama **6,568**(15%) walipata huduma hiyo kupitia hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Rukwa.

**Mheshimiwa Mgeni rasmi**, kwa kuzingatia takwimu za akina mama waliojifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya (**95%**) ikilinganishwa na kiwango cha kitaifa cha 71%,unaona kabisa namna gani wananchi wetu hususan mama wajawazito walivyokuwa na mwitikio mkubwa wa kujitokeza katika vituo vya kutolea huduma kwa lengo la kupata huduma bora za afya.

**Mheshimiwa Mgeni rasmi**, kutokana na idadi kubwa ya mama wajawazito katika Mkoa wetu wanaoitikia wito wa Serikali wa kuhudhuria huduma za kliniki ya wajawazito na kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya, hali hii inaipelekea Sekta ya afya kukabiliwa na changamoto kadhaa kubwa ikiwa ni upungufu wa vifaa na vifaa tiba muhimu na ufinyu wa miundombinu ya kutolea huduma kwa maana ya majengo. Miongoni mwa vifaa hivyo ni pamoja na vitanda vya kujifungulia (Delivery beds), vitanda vya wagonjwa (Hospital Beds), magodoro, mashuka na mipira ya kuvaa mikononi wakati wa kumsaidia mama mjamzito wakati wa kujifungua.Hali hii,wakati mwingine inapelekea akina mama hao kulala chini au kulala zaidi ya mmoja katika kitanda kimoja.

Katika juhudi za kumaliza changamoto hii, Serikali ya awamu ya tano kupitia kwa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt.Jonh Pombe Joseph Magufuli iliamua kuchukua uamuzi wa kununua vifaa vya kutosha vya huduma za uzazi kupitia bohari kuu ya dawa (MSD) kwa ajili ya kuvigawa katika Halmashauri zote Nchini ikiwa ni pamoja na Halmashauri za Mkoa wa Rukwa.

Idadi ya vifaa ambavyo Mkoa umevipokea kwa kila Halmashauri na ambavyo utavikabidhi leo ni kama ifuatavyo;

**Vifaa vilivyokabidhiwa kwa kila Halmashauri**

| Na | Halmashauri | Vitanda vya kujifungulia | Vitanda vya wagonjwa | Magodoro ya hospitali | Mashuka |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Manispaa ya Sumbawanga | 5 | 20 | 20 | 50 |
| 2 | Wilaya ya Kalambo | 5 | 20 | 20 | 50 |
| 3 | Wilaya ya Sumbawanga | 3 | 20 | 20 | 50 |
| 4 | Wilaya ya Nkasi | 3 | 20 | 20 | 50 |
| **Jumla Kimkoa** | | **16** | **80** | **80** | **200** |

**Mheshimiwa Mgeni rasmi**,naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya watumishi wote wa Sekta ya Afya na wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa ujumla kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,kupitia ilani ya chama cha Mapinduzi na kipekee kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Dkt.John Pombe Joseph Magufuli kwa kutimiza ahadi yake ya kuboresha huduma muhimu za uzazi kwa mama zetu wa Mkoa wa Rukwa kwa kutuletea vifaa hivi muhimu vya uzazi ambavyo utavigawa hivi punde.Naomba nikuhakikishie kwamba,vifaa utakavyovigawa leo vitaleta mabadiliko makubwa sana katika ubora wa huduma tunazozitoa na kuzisimamia katika Mkoa wetu

**Kwa nini zoezi hili linafanyika katika Kituo cha afya cha Mazwi**

**Mheshimiwa Mgeni rasmi,** kama ulivyosikia na kuipokea taarifa ya kituo hiki, kwa muda mrefu kituo hiki kilikuwa hakitoi huduma za kujifungua kinyume na Sera ya afya inayotaka huduma zote za msingi zikiongozwa na huduma za afya ya uzazi na mtoto zinazojumuisha huduma za kujifungua zitolewe katika vituo vyote vilivyoko katika ngazi ya vijiji/mitaa (Zahanati) na ngazi ya kata (Vituo vya afya).

Kupitia juhudi za Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, wananchi na wadau wengine ndani ya Halmashauri na kwa kushirikiana na uongozi wa Afya ngazi ya Mkoa,kituo hiki kimeanza kutoa huduma za akina mama kujifungua tangu **tarehe 01 Julai,2017**.

**Mheshimiwa Mgeni rasmi**,ni matumaini yetu kwamba baada ya huduma hizi kuanza kutolewa katika kituo hiki idadi kubwa ya akinamama kutoka katika maeneo mbalimbali ndani nan je ya Halmashauri hii watajitokeza kwa wingi kufuata huduma.Katika kukabiliana na changamoto ya ufinyu wa majengo ya kutolea huduma hizi,umejionea mwenyewe namna ambavyo uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga unavyotekeleza kauli mbiu ya hapa kazi tuu kwa vitendo kwa kukamilisha jengo lingine kwa ajili ya kuhakikisha akina mama wanaendelea kupata huduma bila wasiwasi wowote.

Uongozi wa Mkoa kupitia timu ya usimamizi na uendeshaji wa huduma za afya ya Mkoa utaendelea kuwa karibu na Halmashauri katika kuendeleza juhudi zilizoanzishwa hapa ili kuhakikisha muda mfupi ujao kituo hiki kinaanza kutoa huduma za kulaza wagonjwa wa kawaida na kutoa huduma za upasuaji kwa mama wajawazito wakati wa kujifunguakama Sera ya afya inavyoelekeza.

**Mheshimiwa Mgeni rasmi**, kabla huduma za kujifungua hazijaanza kutolewa katika kituo hiki, huduma hizi zimekuwa zinatolewa katika hospitali teule ya Halmashauri na hospitali ya rufaa ya Mkoa, hali inayopelekea wataalamu walioko katika Hospitali ya rufaa ya Mkoa kutumia muda mwingi kutoa huduma ambazo zingetolewa katika ngazi ya vituo vya afya badala ya kujikita katika kushughulikia matatizo ya rufaa na ya kibingwa.

Kutokana na umuhimu huo,ndiyo maana tulikuomba zoezi la ugawaji wa vifaa hivi vya huduma za uzazi lifanyikie hapa kama njia mojawapo ya kuunga mkono juhudi za uongozi na wananchi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na Mkoa kwa ujumla.Tunakushukuru sana kwa kukubali ombi hili.

**Mheshimiwa Mgeni rasmi,** ninaimani kuwa kwa kituo hiki kuanza kutoa huduma za kujifungua itasaidia kupunguza msongamano wa akina mama katika wodi ya wazazi ya hospitali ya Rufaa ya mkoa na hivyo kuimarisha huduma za rufaa na huduma za kibingwa ndani ya Mkoa.

**Mheshimiwa Mgeni rasmi**, sasa naomba nikukaribishe kwa ajili ya kufanya kutangaza rasmi uzinduzi wa huduma za kuifungua katika Kituo cha afya Mazwi na kugawa rasmi vifaa vya huduma za uzazi katika Mkoa wa Rukwa

Taarifa hii imeandaliwa na timu ya usimamizi na uendeshaji wa huduma za afya Mkoa wa Rukwa na kusomwa na

Dkt.Boniface D.Kasululu

**MGANGA MKUU WA MKOA WA RUKWA**